

WALIMU WA KKK WAMEPEWA MBINU MPYA ZA UFUNDISHAJI

Na. Milka Kaswamila- Bukoba DC

Walimu wanaofundisha darasa la kwanza wameaswa kufanya kazi hiyo kwa moyo na kwa usahihi, huku wakiepuka kutumia darasa la kwanza kama mahali pa kwenda kupumzikia, badala yake, watambue kwamba aibu ya shule huanzia darasa la kwanza ikiwa halitafundishwa ipasavyo, hivyo wawe makini sana wanapokubali jukumu la kufundisha darasa hilo.



Wito huo umetolewa na mwalimu Alex Rwabigene, ambaye ni mwalimu mstaafu na mshahuri wa masuala ya elimu, alipokuwa akitoa mafunzo ya kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), yaliyoandaliwa na Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi, ya Halmashauri ya Wilaya Bukoba, kwa lengo la kuwapa mbinu mpya za ufundishaji na usimamizi wa ufundishaji, kwa walimu wanaofundisha stadi hizo, waratibu wa elimu kata na walimu wakuu kutoka katika shule za msingi za Serikali na zisizo za Serikali za Halmashauri hiyo.

Awali kabla ya kuanza kwa mafunzo hayo, mwalimu Alex alibainisha sababu zinazotajwa kupelekea watoto kushindwa kusoma na kuandika, ambazo ni pamoja na mrundikano wa wanafunzi madarasani na uhaba wa walimu, na walimu nao wakabainisha matazamio yao baada ya mafunzo hayo, kwamba wataweza kupata mbinu bora za ufundishaji na maarifa mapya.



Hata hivyo, katika mafunzo hayo, imeabainika kwamba uhaba wa zana za kufundishia wanafunzi wa darasa hilo na uelewa mdogo wa baadhi ya walimu kuhusu miongozo ya kufundishia ama uzembe wa baadhi ya walimu kufuata miongozo hiyo ndio sababu za msingi zinazopelekea kushindwa kufikia lengo la kufundisha masomo hayo, hivyo wito ukatolewa kwa walimu wote wanaofundisha stadi hizo kuhakikisha wanakuwa na zana za kufundishia pamoja na kuzingatia miongozo ya ufundishaji wa stadi hizo ambayo Wizara ya Elimu imeitoa, kwa sababu miongozo hiyo ni bora na ikiwa itafuatwa vyema italeta matokeo chanya katika ufundishaji na ujifunzaji.

“Mbinu za ufundishaji zilizobainishwa katika miongozo hii zitakapotumika kwa usahihi zitasaidia kuongeza mvuto wa stadi hizo kwa wanafunzi na utoro utapungua pia kwa sababu watoto watafurahia kujifunza na hivyo watapenda kuja shuleni kila siku ili wajifunze zaidi” alisisitiza mwalimu Alex.



Aidha, mwalimu Alex amewashauri walimu wakuu na maafisa elimu kata kuhakikisha wanakuwa karibu na walimu wanaofundisha darasa la kwanza ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo na kuzitatua kwa pamoja huku wakihakikisha wanawapatia zana toshelevu walimu hao ili waweze kufundisha stadi za KKK kwa ufanisi mkubwa.

Miongoni mwa mbinu zilizowasilishwa katika mafunzo haya zitakazoweza kusaidia wanafunzi kujua kuandika na kusoma hata kama kutakuwa na mrundikano wa wanafunzi madarasani ni pamoja na matumizi ya picha, nyimbo na uundaji wa maumbo mbalimbali ya herufi na sauti kwa vitendo.

MWSIHO